

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA THELATHINI NA NNE**

**26 MEI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA NNE – TAREHE 26 MEI, 2023

#### I. DUA:

#### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

##### WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

#### III. MASWALI:

##### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**439. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY  
MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Pensheni za Wastaafu zinalipwa kwa wakati.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**440. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Mradi wa DMDP awamu ya pili utanza kwa lengo la kutatua changamoto ya miundombinu Kigamboni.

**441. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ipo tayari kujenga Kilometa moja ya lami nyepesi Mabila *Station* ili kuboresha mazingira kwa Wafanyabiashara.

**442. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaongeza Watumishi wa Afya katika Hospitali ya Wilaya Meatu.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**443. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, lini Serikali itafanya uhakiki ili kuwarejesha walengwa 2500 waliosimamishwa kupokea ruzuku ya TASAF.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**444. MHESHIMIWA ALEKSIA ASIA KAMGUNA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali imejipangaje kukomesha uvuvi haramu wa kuvua Samaki kwa kutumia nyavu zenye matundu madogo.

**WIZARA YA KILIMO:**

**445. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatafuta suluhisho la kudumu la kudhibiti Wanyama waharibifu wa Mazao na Ugonjwa wa Mnyauko.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**446. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itapitia upya mipaka na kuweka alama za Hifadhi katika Vijiji vya Ndongosi, Mdunduaro, Litumbandyosi na Kiwombi.

**447. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Watalii wangapi walitembelea Mbuga ya Ruaha kwa Mwaka 2019/2020 na upi mkakati wa kuongeza Watalii.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**448. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA  
(MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,  
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Kata za Miyombweni, Malilo, Songwe na  
Luhanga zitawekwa Anuani za Makazi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**449. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Vyuo vya  
VETA katika Wilaya za Liwale, Nachingwea,  
Ruangwa na Lindi Vijijini.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**450. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL KINGU  
(SINGIDA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na  
Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Singida, Sepuka, Ndago hadi Kizaga kwa kiwango cha lami.

**451. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI  
(TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kwa nini ujenzi wa Barabara ya Tarime – Nyamwaga – Serengeti umeanzia katikati badala ya kuanzia Mjini.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO  
YA MAKAZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
26 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**